# F1 TOPICAL REVISION KISWAHILI

***A SERIES OF TOPICAL QUESTIONS IN FORM ONE KISWAHILI***

***FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657***

**MR ISABOKE 0705525657**

# INSHA

## 1.INSHA ZA KIUAMILIFU

1. Andika mahojiano baina ya mkuu wa wilaya na mwandishi wa habari kuhusu utovu wa usalama wilayani mwako.

2. Hali ya usalama imekuwa ikizorota katika lokesheni yako. Andika barua kwa chifu wa eneo lenu ukionyesha visa vya ukosefu wa usalama na upendekeze njia za kukabiliana na hali hiyo.

3. Umealikwa katika ofisi ya mkuu wa wilaya kupendekeza njia za kukomesha uadui unaotokana na ukabila nchini. Andika mazungumzo jinsi yalivyoendelea.

4. Wewe ni kiranja anaye husika na masomo shuleni mwako. Mwandikie kiranja Anayehusika na masomo katika shule jirani ukiwaalika wanafunzi wake katika mjadala shuleni mwako. Ambatanisha ratiba itakayofuata siku hiyo.

5. Andika insha ya mazungumzo ya simu kati ya Kirubi na Ojilo.
6. Safari ni hatua.
7. Tatizo la vijana wanaorandaranda mijini haliwezi kutatuliwa. Jadili
8. Namna ya kupika Ugali.

9.Umeteuliwa kuwa Mwanachama wa Kamati andalizi ya mkutano wa Harambee ya Kuwachangia vilema mkoani mwenu. Tayarisha ratiba itakayofuatwa katika mkutano huo.
10.Bahati ni judi
11.Nchi itaendelea ikiwa elimu itaimarishwa Jadili
12.Ndoto ya ajabu
13.Toa maoni yako kuzishauri serikali za nchi za kiafrika jinsi ya kutumia vyema misaada wanayofadhiliwa na mataifa ya kigeni
14.Mawasiliano yatakavyokuwa mwaka 2100
15.Adui mpende
16.Si lazima kusoma ili kufaulu maishani. Jadili

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

# 2.INSHA ZA KAWAIDA

1. Andika insha itakayotamatika na ....kweli dunia ni mwendo wa ngisi, ina masalata wengi.
2. Elimu bila malipo nchini Kenya ina changamoto zake. Jadili
3. Eleza namna katiba mpya inavyofaa kutetea nafasi na hadhi ya jinsia ya kike.
4. Ajira ya watoto ina madhara mengi. Fafanua.
5. Zigo la kuliwa halilemei.
6. Andika insha itakayomalizikia kwa :
   ….mkuu wa askari aliwaeleza kuwa ikiwa njia hizo zingetumika, uhalifu ungezikwa
   kwenye kaburi la sahau
7. Mwenye kovu sidhani kapoa.

8. Elimu ya bure inayotolewa na serikali katika shule za msingi za umma humu nchini, imekuwa na athari mbalimbali. Jadili.

9. Andika insha itakayomalizikia maneno yafuatayo:-
   ....aliyakumbuka mashauri ya mamake ambayo aliyakaidi. Machozi yalimbubujika alipojiona kadhoofika kiafya jinsi ile; mguu mmoja duniani, mwingine kaburini.

10. Uhaba wa kazi ni tatizo sugu katika nchi zinazoendelea. Jadili.

11. Andika kisa kinachodhihirisha ukweli wa methali: “**subira huvuta heri**”

12. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya:- ...........nilipiga magoti chini na kumshukuru Maulana kwa kuyanusuru maisha yangu.

# UFAHAMU

**1.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Panografia ni tendo, maandishi, picha au michoro inaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, tovuti na kanda za kunasia picha na sauti.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea kote ulimwenguni mithili ya moto mbugani wakati wa kiangazi. Kuenea kwake kumechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi ukiwa umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbalimbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la kuvuruga madili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu.Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Kwa mfano, baadhi ya wanamuziki hutumia **ponografia** kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji wa ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushaihidi kuonyesha kuwa wale wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kwamba kinachoonekana kwa jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kisasi ikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama vile masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera, huyaiga wanayoyaona na kuyasikia. Hii ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Hivyo basi wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa huku wengine wakiambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza kuwaletea mauti.

Yasemekana kuwa akili za binadamu hunasa zaidi mambo yanayowalishwa kwa picha na hivyo basi matusi haya yaweza kudumishwa katika kumbukumbu zao. Tabia mbaya kama vie ushoga, ubasha na usagaji huwa matokeo yake na hata matokeo ya vijana hugeuka wanapoanza kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, lugha, ishara na miondoko inayohusiana nanmgono huibuka. Yote haya yanakinzana na desturi za mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kuchapo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama vile unywaji pombe na matumizi ya vileo ambavyo huchochea uchu wa ngono na kuibua tabia za kinyama.

Kuendelea kuzitazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, huondoa makali kiasi kwamba hata katika uzima mtu hupoteza mhemko na kugeuswa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mjini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na malezi haya yasiyo na kizuizi.

Kuuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi, watu wazima kuwajibika kwa kuwalinda na kuwahimiza vijana kuhusu maovu haya na wale wenye midahilishi, video na sinema kutowaruhusu vijana kutazama uchafu huu kunaweza kuwa maana ya kuyakinga au hata kuyaepuka madhara ya ponografia. Ni sharti pia sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na uenezaji wa upungufu huu. Bila shaka, sheria na hatua kali za ziweze kuchukulia dhidi ya waivunjao. Hali kadhalika, wazazi wasijipweteke tu bali wawaelekeze watoto wao ipasavyo na ila mtu alitekeleze jukumu lake.

**Maswali**

(a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka

(b) Toa sababu za kusambaa kwa uchafu unazozungumziwa katika taarifa

(c) '**Bendera hufuata upepo'**. Thibitisha ukweli wa usemi huu kulingana na makala

(d) Ni kwa nini ni muhimu kuwakanya vijana dhidi ya uchafu huu?

(e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya aina ya uozo unaozungumziwa na mwandishi?

(f) Fafanua msamiati huu kimuktadha

(i) **uchu**

…………………………………………………………………

(ii) **wasijipweteke**

……………………………………………………………….

(iii) **nishai**

…………………………………………………………………

**2.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ilikuwa Jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya Habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za kiinua mgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki.

Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa Kilimo alitangaza

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baaada ya taarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukua mara moja.. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kilimo nilitenga ekari kumu za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikakati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nilipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo ‘amonia.’ Gharama yake ikawa shilingi1,300 kila gunia. Hivyo, nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano..

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siwanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanis wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa ‘Usikate majani, mnyama hajauawa.’

Bila taarifa wala tahadhari mvua ikatoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makasio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi.

Lakini ‘Muumba ndiye Muumbua.’ Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha. Muda is muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tukio lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafhuku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba nikaona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudi hali yake tena, kisha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

ikawa shilingi 5,000. Kuvuna, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa: 'MAHINDI GUNIA 900/=.' Niligutuka usingizini.

**Maswali:**

a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari.

b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika?

c) Taja matatizo **matatu** yaliyotisha mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi.

**d) Eleza maana ya methali zifuatazo:**
(i) Usikate majani, mnyama hajauawa.

e) Eleza mambo **mawili** yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia.

f) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu?

g) **Eleza maana ya:**
(i) kiinua mgongo.

(ii) manyakanga wa kilimo.

3. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Mtoto anapozaliwa huwa ni malaika wa Mungu. Hutaraji kuongozwa kwa kila njia ili awe mwana mwelekea. Jukumu la kulea mtoto huanzia nyumbani. Wako baadhi ya watu ambao wanaamini kuwa jukumu hili muhimu hutekeleezwa bora na mama; wengine husema kuwa ni jukumu la baba. Ni kweli kwamba mtoto huwa na mama yake kwa muda mrefu zaidi ya baba lakini kivuli cha baba hakikosi kumwandama na **kumwathiri** maisha yake.

Uongozi wa mama huanzia siku ya mwanawe kuingia ulimwenguni. Kwa hivyo, mama zaidi ya baba huwa ndiye **chanzo cha chemichemi** ya maisha ya mwanawe. Mtoto kwa kawaida ana tabia ya kuiga kila jambo analoliona na kusikia na mambo ya awali ajifunzayo hutokana na mamaye.

Je; mtoto huiga kutokana na mama pekee? Kila utamaduni hasa huku kwetu Afrika, una taratibu zake zilizopangwa kuhusu malezi ya watoto. Kwa mfano; akina baba wengine wanaoishi maisha ya kijadi huonelea kwamba ni jukumu lao kuwalea watoto wa kiume. Kwa hivyo mvulana anayekulia katika mazingira haya **akishachuchuka** kiasi cha kujua lipi zuri lipi baya huanzia kuwa mtoto wa baba

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

zaidi ya kuwa wa mama. Baba humuathiri mtoto wake kwa kumshauri kuhusu maneno ya kiada ya wanaume. Hupenda kukaa naye katika uga wake kwa kumshauri kuhusu maneno ya kiada ya wanaume huku akimkataza kukaa jikoni na kumsisitizia kuwa wanawake ni tofauti naye. Aidha, humfunza sifa kama vile ushujaa na uvumilivu kwa namna ambayo huona kuwa ni ya kiume. Pindi mtoto anapoonyesha tabia za kikekike, baba hujiandaa kuzitadaruki kwa kumkaripia. Baba hutaka kujiona mwenyewe katika hulka ya mwanawe.

Baba kama huyu humpa nafasi ndogo sana mkewe ya kumwongoza mtoto wake wa kiume kwa jambo lolote hata kama wakati mwingine ni la heri. Kwa upande mwngine baba huyu huwa na machache ya kuzungumza na bintiye kwa kuwa huona kuwa si stahili yake kufanya hivyo. Mtoto wa kike huachiwa mamake. Lakini kutokeapo jambo la kulipima mama huona linampita kimo, humwita baba kuingilia kati na aghalabu baba naye humwagiza dadake aje atoe suluhisho mwafaka.

Ulezi kama huu una nafasi yake katika jamii, lakini ni lazima tukiri kuwa pia unaendeleza maisha ya fawaishi na kuanzisha **taasubi** ambayo hatima yake ni mwanamke kukandamizwa na mwanaume. Wazazi walio na mwelekeo huu katika malezi yao hufikiri kuwa wataishi na watoto wao katika mazingira finyu na kwa hivyo waendelee kuwapulizia pumzi za kuhilikisha. Lakini ni sharti wakumbuke kuwa wao sio walezi peke yao na wala mtoto hawezi kuishi peke yake na kuwa na tabia ya kipekee. Leo ataishi kwao lakini kesho itambidi atoke aone ulimwengu. Kila atakapotia mguu ataona mambo mapya yatakayompa tajriba mpya na mawazo mapya ambayo aghalabu yataendelea kuiathiri **hulka** yake. Iwapo tabia alizozipata kwa wazazi wake hapo awali zilikuwa na misingi isiyokuwa madhubuti na mielekeo finyu, zinaweza kuwa pingamizi katika maingiliano yake na watu wengine. Mambo haya yanatuelekeza katika kufikiri kwamba maisha ya siku hizi hayaruhusu ugawaji wa kazi ya malezi ya namna ya baba na mama wa kijadi. Baba na mama ni walezi wa kwanza ambao kwa pamoja wanapaswa kuwaelekeza watoto wao katika maisha ya ulimwengu uliojaa bughudha na ghururi. Ni lazima wazazi watambue tangu awali kuwa katika malezi hakuna cha ubaguzi. Hakuna, mambo ajifunzayo mtoto wa kiume ambayo hayamhusu mtoto wa kike. Uvumilivu, bidii, utiifu na kadhalika ni sifa zinazomwajibikia kila mtoto kama vile upishi, ukulima na usafi. Mwanamke tangu azali ameumbwa kuwa mama na haipasi kulazimishwa kuchagua baina ya mtoto wa kike na kiume. Mapenzi na wajibu wa wazazi yapaswa yasiwe na mipaka bali yawe maridhawa kwa watoto wote.

**Maswali**

(a) Toa kichwa mwafaka cha makala haya

(b) Kulingana na kifungu hiki, taja mambo **mawili** ambayo yanaweza kuwa hatari kwa malezi ya watoto

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(c) Kwa nini baba humpa nafasi ndogo sana mkewe ya kumwongoza mtoto wa kiume katika jambo lolote hata kama wakati mwingine ni la heri

(d) Eleza mambo **mawili** ambayo ni ya manufaa katika ulezi jadi

(e) Kulingana na makala haya, ushahidi gani unaonyesha kwamba kuna kutegemeana katika ulezi jadi?

(f) Taja sifa **mbili** ambazo baba humfundisha mwana wa kiume

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kaktika kifungu hiki:

(i) **Chanzo cha chemichemi**...

(ii) **Akishachuchuka**...

(iii) **Hulka**.

***4. Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Habari kuwa watoto chini ya miaka mitatu <u>‘huwindwa’ kitandani</u> na kuraushwa na wazazi wao waende shuleni mwendo wa saa kumi na moja asubuhi ni za kusikitisha.

Kwa mujibu wa ripoti za wataalamu wa elimu ya watoto wachanga (ECD), watoto hao hutakikana kuwa darasani kabla ya saa kumi na mbili asubuhi.

Wanapowasili wao huanza kufukuza ratiba ya masomo ambayo huwapatia muda mfupi mno wa kula, kucheza, kupumzika na hata kuchunguza afya na usalama wao.

Badala ya kuondoka mapema kuelekea nyumbani, wengi wao hufika saa za usiku pamoja na wazazi wao wakitoka kazini. Wanapowasili nyumbani wanapaswa kuoga na kupata chakula cha jioni kwa pupa ili wafanye mazoezi waliyopewa na walimu wao.

Mazoezi hayo huwa ya masomo yote matano huku kila somo likiwa na zaidi ya maswali thelathini. Badala ya kupumzika mwishoni mwa juma, watoto hao huhitjika kuhudhuria shule siku nzima ya Jumamosi. Jumapili wanatakiwa Kanisani na hali hii hujirudia mpaka muhula umalizike. Ikiwa ulidhani watapewa nafasi ya kupumzika wakati wa likizo , umekosea kwa sababu watoto hao huhitajika kuhudhuria shule. Hili limekuwa likiendelea hata baada ya Wizara ya Elimu kupiga marufuku kusomesha wakati wa likizo.

Wazazi-hasa wale wanaofanya kazi mijini- wamekuwa wakiunga mkono mtindo huu kwa sababu unawaondolea mzigo wa malezi na gharama ya kuwaajiri walezi.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Wataalamu wanasema matokeo ya hali hii ni watoto **wakembe** wenye afya na **maadili** mabaya kutokana na kuchanganyishwa akili na walimu wanaowataka wajue kila kitu wakiwa na umri mdogo.

**Kuwashinikiza** watoto wakembe wahudhurie shule na zaidi ya hayo wajue kila kitu kuna madhara mengi. Kwanza kabisa, kuraushwa kwa watoto macheo waende shule kunawanyima fursa ya kulala na kupumzika. Utafiti unaonyesha kuwa watoto wanahitaji kulala na kupumzika kwa zaidi ya saa 12 kwa siku. Hii ina maana kuwa mbali na muda mfupi wanaolala na kupumzika mchana kutwa, watoto wanapaswa kutumia usiku mzima kwa usingizi.

Hii huwasaidia kukua wakiwa na afya nzuri hasa kiakili. Matokeo ya kuwarausha watoto hao waende shule saa hizo huwafanya wakose furaha mbali na kuwafanya wachanganyikiwe kiakili.

Pili, kuwalazimisha watoto wakae darasani kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni huwa kunawanyima fursa ya kucheza na kutangamana. Wataalamu wa afya ya watoto wanapendekeza kuwa watoto wachanga wanapaswa kucheza ili viungo vya miili yao kama moyo, akili, mapafu na kadhalika vifanye kazi vizuri.

Kinyume na watu wazima ambao hufanya kazi nzito nzito na kuwawezesha kufanya mazoezi, watoto huwa hawafanyi kazi hizo. Wazazi na walimu wanapaswa kufahamu kuwa kazi ya watoto ni mchezo na wana kila haki ya kupewa furaha ya kucheza wakiwa shuleni na hata nyumbani.

Tatu, wazazi wengi ambao hufurahia kuwaachia walimu jukumu la kuwalea watoto wao huku wao wakiwa kazini huwa wanasahau kuwa sio kila mwalimu ana maadili yanayopaswa kuigwa na mwanawe. Ingawa tunawatarajia walimu wawe mifano bora ambayo inaweza kuigwa na kila mtu, ukweli ni kwamba baadhi ya walimu hawajui maana wala hawana maadili. Hatari ni kwamba watoto **wakembe** husoma kwa kuiga wakubwa wao na ikiwa walimu wanaoshinda nao shule wamepotoka kimaadili, kuna uwezekano mkubwa wa watoto hao kupotoka pia. Hii ndiyo sababu wazazi wengi wamekuwa wakilalamika kuwa wanawao tabia mbaya ambazo hawaelewi zilipotoka.

Kila mzazi anayejali maisha ya mwanawe anapaswa kutekeleza jukumu lake la kumlea na kumwelekeza jinsi anavyotaka akue. Ni kinaya kuwa wanawatarajia wanawao wawe na tabia na maadili kama yao ilhali hawachukui muda wa kukaa nao na kuwaelekeza.

Nne, kuwawinda, kuwaamsha, kuwaosha na kuwalazimisha watoto waende shule kila siku hata ingawa hawataki huwa kunawafanya wawe wategemezi wasioweza kujipangia na kutekeleza mambo kivyao.

***(TAIFA LEO, IJUMAA, FEBRUARI 5, 2010)***

**MASWALI.**

(a) Ipe taarifa anwani mwafaka

(b) Mwandishi anatoa maoni gani kuhusu ratiba ya masomo?

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(c) Eleza athari za mfumo wa elimu unaoangaziwa hapa

(d) Ni ushauri upi unaotolewa kwa wazazi ?

(e)Taja mbinu zozote **mbili** za lugha alizotumia mwandishi

(f) Eleza **maana** ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa.

(i) '**huwindwa' kitandani**

(ii) **Maadili**

(iii) **Kuwashinikiza**…

(iv) **Wakembe**…

## 5. UFAHAMU

Nchi zetu za Afrika zinakumbwa sana na ukosefu wa mvua. Inasemekana ya kwamba jangwa linazidi kutanda katika bara hili, kwa hivyo ni wajibu wetu kujiandaa na kuchukua hatua kadha wa kadha ili tuweze kupambana na ukavu huu, kwani wahenga walisema, "Uwahi udongo uli maji."

Kwa hakika ukavu huu unasambaa katika bara hili na unatutia hofu kubwa. Imekuwa sana tunategemea nchi za kigeni kutusaidia. Tukichunguza zaidi sababu kubwa ya ukosefu wa mvua ya kutosha ni ukataji wa miti. Kwa hivyo tuhakikishe kuwa tutapanda miti kwa wingi wakati wa mvua. Serikali ya Kenya inahimiza sana upandaji wa miti katika sehemu mbalimbali za nchi. Pia lazima tuhakikishe kwamba baada ya mche kupandwa, kufanywe mipango na kupatikane watu ambao wataiangalia na kuipalilia hadi itakapokuwa mkubwa. Ni wazi kwamba tumetilia mkazo wa kupanda miche lakini hatujazingatia miche hii kuangaliwa kwa kunyunyiziwa maji wakati wa ukame.

Hatua ya kuchimba visima, katika sehemu zenye ukavu ni jambo la muhimu sana, kwani maji ya visima yataweza kutumika majumbani na pia kunyunyizia mimea. Maji kwa binadamu ni kitu muhimu sana kwa sababu bila ya maji hakuna uhai. Huko Australia, visima vingi vimechimbwa katika sehemu zenye ukame kwa minajili ya kuwapatia wakazi wa sehemu hizo maji ya nyumbani, mifugo na kunyunyizia mimea.

Maji ya mvua na yale yanayochuruzika mitaroni, hukusanywa na kutumiwa kwa kunyunyizia mimea. Mashamba yanayonyunyuziwa maji ya aina hii, hunawiri na kustawi sana. Maji ya mito ambayo huchuruzika baharini, lazima tuyatumie baada ya kuiondoa chumvi ndani yake. Vile vile, tujaribu tuwezavyo kupanda mimea ambayo itatupa chakula cha kutosha ili tuweze kujitegemea badala ya kuzitegemea nchi za kigeni.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(a) Mwandishi ametumia methali "uwahi udongo uli maji" akimaanisha nini hasa? *(alama 3)*

(b) "Haitoshi tu kupanda miche na kutulia". Kulingana na yaliyomo katika taarifa hii, ni hatua gani zingine zinazohitajika ili kufaulu katika mradi huo wa upanzi? *(alama 3)*

(c) Taja jitihada zozote mbili zinazochukuliwa na serikali ili kukabiliana na shida ya ukosefu wa mvua / maji*(alama 4)*

(d) Kwa nini maji ya baharini hayatumiwi moja kwa moja? *(alama 2)*

(e) Kwa nini nchi nyingi za bara la Afrika zinategemea nchi za kigeni? *(alama 3)*

(f) Maneno yafuatayo yametumiwa kuleta maana gani? *(alama 5)*

(i) Kutanda_______________________________________________

(ii) Miche_______________________________________________

(iii) Kunyunyizia___________________________________________

(iv) Hunawiri___________________________________________

(v) Kustawi____________________________________________

## 6.UFAHAMU

Thamani ya shilingi ; tokea ibuniwe kama sarafu ya kuendesha biashara, inadunika kila kukicha. Tukirudisha nyuma gurudumu la wakati tutaweza kuchungulia na kujionea mengi ambayo yalikuwa yaweza kununuliwa kwa uwezo wa sarafu moja tu ya shilingi. Fungu la machungwa, au mkungu mzima wa ndizi au tita la kuni – haya yote yalikuwa yaweza kulipiwa shilingi tu kabla ya kumiliki kama mali yako. Kweli zama hizo, shilingi ingeweza kukushibisha na usilale na njaa.

Shilingi yenyewe ilikuwa na miujiza mingine. Thamani yake kwa miaka na miaka, ilikuwa ni ile ile na athara kama vile za kuanguka kwa thamani ya pesa ilikuwa ni jambo geni kabisa katika janibu hizi. Kwa wengi wa wakazi wa huku, athari hizo za kuanguka kwa thamani ya shilingi au Sarafu zozote zile za kilimwengu kama vile dola thabiti, yalikuwa ni matukio ambayo yalijulikana huku kama ndoto za vitabu vya historia tu. Ndoto hiyo leo ni ukweli mgumu usioaminika. Hali imewia kuwa ngumu zaidi na shilingi imekuwa chepechepe na ni shida kuitumainia kukunufaisha kwa chochote kile ila ukiwa na uraibu wa sigara moja mbili au ukiwa wataka kununua pipi tatu kwa kuondoshea ukakasi unaotokana na kuvuta sigara.

Shilingi 'haingiari ikaua' Enzi hizo zimepita na kamwe hazitarudi tena. Leo mifumo mbalimbali ya kiuchumi duniani imo katika gharika kweli kweli kwani adui 'inflesheni' amefaulu kuzizorotesha na kuziacha katika hali dhaifu viongozi mbali mbali kote duniani wakitawazwa, tamko lao la kwanza ni kupambana na adui huyu na kuingia katika utawala wao na kujitolea kupambana naye adui huyo kama yumo katika vita vya kufa na kupona.

Uchumi mwingi umenyauka. Fikira na wataalamu wengi wenye kufahamu sayari ya uchumi wangali wamekaukiwa na mbinu za kumwagusha adui huyo ili maisha yarudie ile hali ambayo ilikuwa yadumu kila mahali ulimwenguni. Vitabu vya historia havisaidii kitu kwani fani yake adui huyu ilikuwa bado haija wakumba binadamu.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Usawazishaji wake 'inflesheni' wategemea mawimbi ya thamani za sarafu maalumu za kilimwengu. Wakati zinapokuwa makini na hazianguki kutokana na thamani zake, biashara na thamani ya shilingi zetu huwa pia shwari na zenye kurahisisha uendeshaji na upangaji wa biashara. Lakini mawimbi yake yakianza kugharikisha thamani za sarafu hizo, shilingi nayo huwa kama yalewalewa katika bahari ambayo haina upeo.

**Maswali**

a) Toa tofauti mbili baina ya shilingi ya zamani na ya sasa ( alama 4 )

b) Mwandishi wa taarifa hii alichochewa na nini hasa hadi akaandika ? ( alama 3 )

c) Kuna ithibati gani kutoka taarifa kuonyesha kuwa kuanguka kwa thamani ya shilingi ni tatizo kubwa duniani ? ( alama 4 )

d) Mwandishi ametumia jazanda nyingi ili kusisitiza unyeti wa swala hili; kwa mfano … tukirudisha nyuma gurudumu la wakati……… taja na uelezee jazanda nyingine zozote mbili na uelezee maana ya kila moja ( alama 4 )

e) Kuna faida gani thamani ya sarafu maalumu ulimwenguni inapokuwa thabiti ? Toa ithibati zako kutoka taarifa ( alama 2 )

f) Eleza maana ya maneno haya kulingana na muktadha wa taarifa hii ( alama 3 )

i) Inflesheni

ii) Janibu

iii) Mawimbi

## 7.UFAHAMU

Yaonekana watu hawajali usanifu wa Kiswahili katika Afrika Mashariki kwa sababu hakuna chombo chenye uwezo wa kutoa uamuzi kuhusu istilahi na matumizi ya lugha. Katika Mashairi na tungo zingine umepenya katika riwaya na unazusha tisho kubwa kwa Kiswahili sanifu. Maneno Kama vile kua, tua, sikia na lia huandikwa na wengi kana 'kuwa, tuwa, sikiya na liya.'

Matumizi ya lugha isiyo sanifu kama haya yaweza kuvumilika yakiwa katika lugha ya mazungumzo au ya mashairi. Maandishi sanifu na wastani yanatakikana kusisitizwa. Kukosa kutumia mtindo mmoja wa kuandika maneno ya Kiswahili kunazusha mawazo kwamba kila moja yuko huru kuandika kiswahili vile apendavyo. Ikiwa tunafanya bidii kuandika maneno ya kiingereza kama vile 'saw', 'sew', 'sow' na 'soul' kwa kutumia irabu inayotakikana ni kitu gani kinachotushawishi kuandika 'sikiya' badala ya 'sikia'? Tunahitaji chombo chenye uwezo katika eneo zima la ulimwengu wa kiswahili ili kusuluhisha masuala kama haya.

Baadhi ya watu wanaweza kuwa na hofu kwamba kuanzishwa kwa Kamati au Baraza kama hilo kutaweza kuhatarisha hali ya kiingereza katika Afrika Mashariki, hasa katika Uganda na Kenya. Hofu kama hiyo haipaswi kuwepo kwa sababu kama nilivyoelezea, kusaidia matumizi ya kiswahili sanifu hakuizuii nchi kufuata sera ya lugha inayopendelea kiingereza vile vile ni wazi kwamba kiingereza si lugha ya Uganda, Kenya au Tanzania. Katika Afrika Mashariki kiingereza kitabaki kuwa lugha ya kigeni yenye umuhimu wa mawasiliano ya kimataifa na maandishi ya kitaaluma. Afrika Mashariki itaendelea kutumia

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

kiingereza katika elimu ya juu na kuiwezesha kunufaika na maandishi ya kitaaluma na kiufundi.

**MASWALI**

(a) Pendekeza anwani mwafaka kwa taarifa hii? (alama 2)

(b) Kwa nini mwandishi anaona kuwa Kiswahili hakitiliwi maanani katika Afrika Mashariki? (alama 4)

(c) Kinachohitajika ili kiswahili kiweze kuimarika ni nini?

(c) Ni jambo gani hasa linalomshawishi mwandishi kuona kuwa Kiswahili sharti kiimarishwe? (alama 3)

(e) Unafikiri kilichochangia udunishaji huu wa kiswahili ni nini? (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyotumika katika taarifa (alama 4)

(i) Usanifu

(ii) Umepenya

(iii) Sera

(iv) Kielelezo

**8.** **(UFAHAMU)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Ama kweli maishaya vijana wa kisasa yanatofautiana na kuhitilafiana pakubwa na yale ya wazee wao. Sio katika mavazi, mienendo, mitazamo, mawazo na mielekeo tu ball pia katika kipengele kingine chochote utakachofikiria. Yote haya ni vielelezo vya jinsi *kizazi* cha leo kinavyoishi katika ulimwengu ambao ni kivuli tu cha ule wa vizazi vilivyotangulia. Baadhi ya watu wameieleza hali hii kuwa maisha sio jiwe. Kwao basi, si ajabu katu kuwaona vijana wakizungumza lugha yao ya kipekee au wakivaa nguo zinazobana ajabu na kudhiirisha bay ana maungo yao badala yakuyasitiri.

Hata hivyo, watu wengi wameonelea kwamba hali ya maisha ya vij ana wa leo ni maasia yanayotokana na utundu na hata ukatili wao. Upande huu umetoa rai kwamba *kizazi* hiki kisingepotoka kama tu kingezingatia na kustahi utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimokulia. Wanazidi kufafanua kuwa nyendo hizi za miaka ya nyuma zilithamini sana amali kama uaminifu, heshima kwa wazee ama wakuu, bidii, ushirikiano, ukarimu, unyenyekevu, hadhari katika kiia jambo, utiifii na pia kujitegemea. Yote haya yamesahaulika ama tuseme yamepuuzwa katika "utamaduni wa kisasa".

Swali linalozuka sasa ni je, tunapaswa kuwahukumu vijana wa leo kwa kutumia vigezo au masharti gani? Tuwapige darubini kwa kutegemea hali ili vyo hivi leo duniani ama tuwapime kwa muj ibu wa j insi maisha ya baba na babu zao yalivyokuwa. Jibu la swali hili ni gumu na sharti lifafanuliwe kwa makini lisije likaegemea upande wowote.

Mathalan, ni jambo lisilopingika kuwa maisha ni utaratibu unaothirika na hi vyo kubadilika daima. Angalia kwa mfano jinsi maendeleo ya elimu, sayansi, mawasiliano na hata

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

ufundi yalivyoyageuza maisha siku hizi. Yamkini vijana wa barani Afrika wakaona na hata kuzungumza kwa wenzao kutoka Uropa, Asia na Marikani bila hata kimyanyuka hapakwao nyumbani. Athari ya filamu, video, vitabu, magazeti, majaridan!k. haikadiriki. Kiasi yamewafanya vijana hata kupevuka kabla ya wakati wao. Isitoshe, mambo haya yameweza kuwazuzu; kuwaaminisha kuwa yale wanayojifunza ni kweli. Matokeo yamekuwa ni wao kuudunisha utamaduni wao wa asm na kuupapia ule wa wageni waiiowaathiri. Tusisahau kuwa ujana ni tembo la mnazi na rahisi kwao kubadili mawazo.

Lakini hatuwezi kuwasamehe vijana wanaokosa akiii razini kwa kupotoshwa na kucharika na yote wanayoyapokea kutoka ugenini na hivyo kuanza kudhalilisha utamaduni wa Waafrika. Hata hivyo, badala ya kiiwakashifu wanapotea njia ama kuwapongeza wanapotenda yale tunayoyategemea tu ni wajibu mkubwa wa wʳazazi kuwaongoza na kuwasaidia vijana kuwa na uwezo mkubwa na kufanya uteuzi mwafaka katika maisha yao.

**Maswali:**

(a) Kulingana na mwandishi, kundi linalodai kuwa 'maisha siojiwe'linamaoni gani?

(alama 2) (b)

Kulingana na taarifa uliyoisoma ni jinsi gani vijana wa kisasa wangeziepuka

athari mbaya. (alama2)

(c) Kwa mujibu wa taarifa hii, utamaduni wa Kiafiika una manufaa.Yataje.

(alama 4)

(d) Mwandishi anaposema Mambo haya yameweza kuwazuzua na kuwaaminisha vijana kuwa yale wanayojifunza ni kweli anamaanisha nini? (alama 4)

(e) Mbalina wazazi, mmakundiganimengineya watu

Ambayo yanapaswa kutoa mawaidha kwa vijana? (alama 3)

(f) Kwa maoni yako vij ana wanapas wa kufanya uteuzi wa namna gani katika m

vutano him wa tamaduni ? (alama2)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(g) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotiimiwa katika makala .

i) maasia

ii) razini (alama2)

h) Andika methali moja ambayo inaafiki taarifa hii (alama 1)

**9.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Zamani sana na hata hivi karibuni watii wengi wote duniani walikuwa wakiamini kuwa kuna ardhi na mbingu tu basi. Imani hii ilijikita katika mantiki yanayosema kwamba ardhi au dunia ipo katikati ya maumbile yote na isitoshe, ni tamb^rare.

Juu ya ardhi ni mbingu ambayo imejaa vimulimuli vidogo vidogo sana viitwavyo nyota. Baina *ya* vimulimuli hivyo vipo viwili vikubwa viitwavyo mwezi na jua. Hivi viwili japo ni vikubwa kuliko vile vingine, bado ni vidogo kuliko ardhi.

Hii ndiyo imani iliyoutawala ulimwengu kwa miaka na mikaka, na ikawa imekita mizizi. Lakini jinsi wanajimu walivyozidi kuelimika, waligundua kwamba ukweli wa mambo umejitenga kando kabisa na imani hii.

Ukweli wenyewe ni kwamba bwaka zima tulionalo la rangi ya samawati nusumviringo juu ya paaa zetu za vichwa ni kubwa sana tena. Nasi kubwa tu bali lazidi kupanuka. Katika bwaka hili lipanukalo kila uchao mna galaksi nyingi ajabu zisizokadirika. Ndani ya kila galaksi mna nyota mamilioni na mabilioni, malaki na kunui. Imejulikana kuwa nyota hizi, japo huonekana kama vimulimuli vidogo sana usiku usiku ni kubwa ajabu. Kadiria mwenyewe! Jua letu ni nyota kubwa sana. Ukubwa wake umezidi wa dunia yetu mara nyingi sana, zaidi ya elfu moja! Basi fikiria juu ya ukubwa wote huo. Imegunduliwa ya kwamba jua ni nyota ndogo sana ikilinganishwa na zingine zilizo katika galaksi yetu tu, lichaya galaksi nyinginezo zilizoko katika bwaka.

Na haya sio maajabu peke yake. Wataalam wamevumbua mengi ya kushangaza zaidi. Mathalan, imekuja kufahamika kuwa jua letu ambalo ni nyota, lina sayari tisa zinazolizunguka. Baadhi ya sayari hizi ni Ardhi yetu, Zaibaki, Zuhurua, Miiihi, na Mshitara baina ya tisa jumla.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Baadhi ya sayari hizi zina visayari vidogo vinavyozizunguka. Visayari hivi ndivyo viitwayo miezi. Ardhi yetu ina mwezi mmoja tu ambapo sayari nyingine zina zaidi ya hesabu hiyo. Kwa mfano, Mirihi ina miezi miwili ilhali Mshitara ina kumi na miwili ! Sayari hizi zote na visayari vyao, au vitoto ukipenda, havitoi mwanga. Num ya mwezi, na nuru ya hizo sayari zinazolizunguka jua letu inatokana na jua lenyewe. Kwa hakika ni mmeremeto tu unaotufikia sisi kupitia sayari hizi kutoka kwa nyota hii yetu iitwayo JUA.

Kama wasemavyo waswahili, ya Mungu ni mengi. Taswira tuliyo nayo katika maelezo hayayaonyesha jinsi ambavyo mwanadamu, licha ya kuwa na akili nyingi, bado hajawahi kuigusia siri kamili ya Mungu. Lakini kwa uflipi twaweza kusema hivi. Ikiwa katika bwaka lote kuna galaksi nyingi, bila shaka kwa vile jua ni nyota, basi zimo sayari nyingi ajabu zinazozunguka kila nyota au jua kama zipasavyo kuitwa. Kwa vile katika mfumo-jua wetu imo sayari moja yenye viumbe vyenye uhai, binadamu wakiwemo, basi bila shaka katika mifumo-jua mingine katika galakasi yetu zipo sayari zinazofanana na ardhi hii yetu, ambazo zina viumbe vilivyo hai... penginepo watu pia! Waona maajabu hayo? Na katika magalaksi mengine je? Mambo pengine ni yayo hayo! Kwa hivyo huenda ikawa hatumo peke yetu katika bwaka hili; labda tuna viumbe wenzetu ambao hatutakutana nao katika uhai wetu kwa sababu ya uwezo wetu na kimaumbile, na vile vile wa kisayansi, ni hafifu. Lakini, kwa vile mwenye kupanga maajabu hayo yote, yaaani Mwenyezi Mungu ni huy o mmoj a basi huenda sote tukakutana Ahera.

Mungu ni mkubwa.

(a) Kulingana na habari hii, taja mamo manne ambayo ni imani potovu (alama 4)

(b) Kwa kusema "ukweli wa mambo umejitenga kando" mwandishi anamaanisha nini? (alama 2)

(c) Taja sifa zozote nne za maumbile ya anga zinazopatikana katika habari hii (alama 4)

(d) Taja vitu viwili vipatikanavyo katika galaksi (alama 2)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(e) Taja sayari mbili ambazo ni kubwa kuliko Ardhi (alama 2)

(f) Ni ithibati gani iliyotolewa kuonyesha kuwa nyota sio vijitaa vidogo?

(alama 2)

(g) Bainisha nuru aina mbili tuzionazo angani (alama 2)

(h) i) Ni neno gani lenye maana sawa na "anga" ama "upeo" katika habari hii?

(alama 1)

ii) Andika neno moja ambalo Una maana sawa na paa kama lilivyotumiwa katika taarifa. (alama 1)

(i) Mwandishi anaposema kuwa katika magalaksi mengine "mambo pengine ni yayo hayo" anamaanisha nini? (alama 1)

**10.UFAHAMU**

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

***Soma habari if uatayo kisha ujibu maswali***

Binadamu kwa wakati huu amemaka kwa sababu amechafua mazingira yake pasipo tahadhari. Mathalani insiya amejaza gesi za sumu zitokazo viwandani na hata kuchafua mito kutokana na maji machafu kutoka viwanda hivyo. Takataka zinazpotupwa ovyo ovyo zinarundikana kila mahali. Isitoshe miti inakatwa vivyo hivyo bila simile.

Matokeo ya haya yote ni kwa mfano tunapata mvua ya asidi ambayo huhasiri mimea. Aidha na ukanda wa ozoni unaotukinga dhidi ya miali hatari kutoka kwa jua umeharibiwa tayari na hivyo kuongeza joto duniani. Sehemu nyingi zimeanza kugeuka na kuwa jangwa huku sehemu zingine zikifurika kwa maji ya mito na mvua. Maji haya yameanza kumeza visiwa vingi vilivyo baharini. Kutokana na madhara haya, binadamu sasa anatapatapa ili kutafuta makao kwingine kwenye salama. Ndiposa siku hizi nadhari za binadamu zimeelekezwa katika mawanda mengine nje kabisaya kisayari hiki kidogo kiitwacho dunia.

Kwa miaka mingi sasa binadamu amekuwa akitafakari uwezekano wa kuishi katika sayari nyingine. Hii ndiyo sababu mwaka wa 1969 Waamerika walimkanyagisha binadamu wa kwanza kabisa mwezini. Lengo lilikuwa ni kutalii na kuchunguza uwezekano wa binadamu kuishi huko ili wale watakaoweza wahamie huko. Kwa bahati mbaya iligunduliwa kwamba mwezini hakuna hewa wala hakuna kilicho hai huko, hata mimea. Mwezini ni vumbi tupu lisiloota chochote. Kipatikanacho kwa wingi sana ni madini tu, ambayo hayawezi kumfaidi binadamu kwalolote.

Sayari nyingine alizozitalii binadamu ni Zuhura, Mirihi, Mushtara na tuseme karibu zote zinazolizunguka jua. Kilichogunduliwa ni kuwa upo uwezekano wa sayari kama Zuhura na pengine Mirihi kuwa na mvua, lakini nyingi mno isiyoweza kuruhusu mimea kukua. Si tu, Zuhura inasemekana kuwa joto sana wakati wa mchana ilhali Mirihi ni baridi sana siku zote; baridi kiasi cha kuwa binadamu na wanyama hawawezi kuishi huko. Mushtara yasemekana kuwa joto ajabu, ambapo hizo sayari nyingine zina joto sana au zina baridi sana. Habari hii imemfunga binadamu katika jela ya kijisayari chake kiki hiki kiitwacho dunia anachokichafua kila uchao.

Je, binadamu amekata tamaa? Hata kidogo! Ndio mwanzo anaj aribu sana kuzikata pingu alizofungwa na maumbile. Vipi? Amejaribu kuchunguza uwezekano wa kuihama ardhi na kuishi baharini, kwa sababu bahari inazidi ardhi mara tatu kwa ukubwa. Na ni vipi binadamu anadhani anaweza kuishi baharini mahali ambapo hakuumbwa aishi humo kama samaki? Jawabu ni kuwa angefanya hivyo kwa kutumia maarifa yake.

Binadamu anaamini kabisa kuwa na uwezo wa kuj enga mij i mikubwa humo humo baharini.... mikubwa zaidi ya hii tuliyo nayo ardhini. Anaamini ya kuwa anaweza kuitawala bahari kiasi alichoitawala ardhi, na hivyo basi kufanya bahari impe makao na kumlisha bila ya kuyabadilisha maumbile yake. Na iwapo hili halitawezekana basi, ikiwajibika, abadilishe maumbile yake kwa kujiunda mashavu kwa mfano, ili avute pumzi ndani ya maji.

Njia ya pili ya kuepukana na pingu za maumbile ni kuishi angani. Hii ina maana ya kujenga miji iliyoelea angani, kama madungu vile. Na kwa vile anga haina kikomo9 binadamu

atakuwa amejipatia nafasi kubwa ya kuishi bilakujali ongezeko laidadi yake mwenyewe. Yaani atakuwa amejiundia visayari vyake visivyo idadi angani!

Njia ya tatu ni kubadilisha umbo lake ili asihasirike na joto wala baridi. Binadamu wa ki sasa anaamini kuwa inawezekana kumuunda upya mtu katika maabara badala ya kutika mimba. Mtu huyu wa maabara, aitwaye 'Cyborg' kwa lugha ya Kiingereza, anaweza kuwa na chuma ndani, badala ya mifupa, na mwili wa kawaida wa dongo na maji nje.

Kiunde huyu atakuwa hadhuriki ovyo ovyo kama binadamu wa sasa aliyeumbwa kwa chumvi, maji na protini. Au bora zaidi, binadamu mpya wa maabarani aundwe kwa zebaki. Binadamu huyu wa zebaki hafi wala hakatikikatiki. Na iwapo atakatika vipande vipande, b isi, kama zebaki, vipande hivyo viaundika tena upya na kumrudhisha umbo la awali kamili.

Njia nyingine ya kuepukana na uangamizi ni kutumia viunde vyake vya elektroniki kama vile tai uidlishi yaani kompyuta, na mitambo mingine kama hivyo. Binadamu anaamini kwamba uwezo wa vyombo hivi vitapokamilishwa, basi vitamsaidia

kwa lolote lile.

**Maswali:**

(a) Inasemekana kwamba binadamu anakichafua hiki kisayari chake kila uchao.

Kwa kutumia rnifano mitatu, eleza vile binadamu amechafua mazingira yake.

(alama3) (b)

Kwa nini ongezeko la joto limeleta janga duniani na wakati huo.huo likaleta

mafuiriko. (alama3)

(c) Eleza sababu mbili zinazomfanya binadamu kuhangaikanakutafuta makao

kwingine. (alama2)

(d) Ni mambo gani yanaofunga binadamu katika ardhi. Taja mawili (alama 2)

(e) Unadhani ni kwa nini madini mengi yaliyoko mwezini hayaletwi duniani. Taja na

ufafanue sababu mbili. (alama4)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(f) Kulingana na aya mbili za mwisho, eleza jambo ambalo binadamu anajaribu

Kukwepa (alama2)

(g) Eleza maaana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu.

(alama4)

i) Mashavu..........................................................................

ii) Madungu………………………………………………… iii)
Asihasirike…………………………………………………..

iv) Kiunde..........................................................................

# 11.UFAHAMU

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata***

Kuna sayansi mpya inayoitwa "cloning" kwa lugha ya Kiingereza. Pengine kwa sasa tuiite "kutumbisha". Sayansi hii tayari imeleta mapinduzi makubwa katika uzaiishaji mimea na uvunaji. Imesemekana ya kwamba, ghairi ya wivu na .kij icho baina ya jamii mbalimbali ulimwenguni,

aina hii ya sayansi ina uwezo wa kuangamiza kabisa janga ia njaa katika say ari hii yetu. Kivipi? Rahisi kabisa. Ni kwamba mbegu moja tu ya aina yoyote ya mmea, baada ya kuneemeshwa, vyumba vyake vidogo vidogo ambavyo ndivyo hasa msingi wa uhai vinaweza kunyunyiziwa dawa maalum ili vitawanyike mara hata mamilioni na kuwa mimea kamili................ mamilioni!

Sayansi hii tayari inatumiwa kukuza viazi na vyakula vingine. Hii ina maana ya kwamba rnasharnba makubwa makubwa si muhimu siku hizi, yaani vyakula vingi kabisa vinaweza kukuzwa mahali padogo sana. Kwa hivyo hivi karibuni tu, kutakuwa hakima haja ya kuigania mashamba.

Vyema. Hebu sasa tuangalie zilizokwishapigishwa hii sayansi ya "kutumbisha na mahali binadamu alipofika kimaendeleo kwa sababu ya hatua hizo. Jambo la kwanza sayansi hii tayari imeshatumiwa kuzalishia wanyama  wengi sana wadogo wadogo kwa lengo la kuendeleza mbele utafiti. Kufikia sasa, wanyama hawa waliotengezwa na binadamu katika maabara yake bado wanahifadhiwa mumo humo walimotengenezewa. Hii ni hatua kubwa na binadamu anastahiki pongezi kwajinsi anavyotumiaakili yake kuvumbua ibura hizi zote.

Hata hivyo imesemwa kwamba <u>kuchamba kwingi ni kuondoa mavi</u>. Binadamu kama ijulikanavyo, anajaribu sana kujitakasa kwa kujitenga mbali sana na asili yake ya unyama ili aufikie ubinadamu mkamilifu. Hapana ubaya hapo. Lakini tukirudi nyuma tunakuta ya kwamba binadamu sasa ameingia tamaa kubwa sana binadamu ana jua vizuri sana kwamba kwa vile ana ujuzi wa kutengeza panya na hata kondoo katika maabara basi hata ujuzi wa kutengezabinadamupiaanao! Nahapo ndipo tatizo lilipo. Swali ni hili: Je?

ujuzi huu utatufikisha wapi?Nakikomo chake kitakuwaje?

Binadamu sasa ujuzi wake unamtia wasiwasi. Wataalam wa sayansi hii wamejiuliza mara nyingi nini kitakachotokea ujuzi huu utakapomilikiw na"mwenda wazimu mweledi." Watu kadha wa kadha, miongoni mwao wakiwa wanasiasa wamejiuliza mara zisozohesabika swali hili: kama Hitler angekuwa na ujuzi huu, angekuwa na lazima gani ya kuwaulia mbali Wayahudi milioni sita wasiokuwa na hatia isipokuwa ya kwamba walikuwa na mij ipua mikubwa, hawakuwa na macho ya buluu, walikuwa na nywele nyeusi na hawakuwa weupe sana kama Wazungu? Hitler alimamini ya kwamba "mtumzuri" ni mwenye pua ya upanga (kama Mzungu), macho ya buluu, nywele rangi ya dhahabu na mwenye kimo cha futi sita au zaidi kidogo. Hivyo lengo lake lilikuwa ni kubuni taifa la watu wazuri pekee ambao mwisho watautawala ulimwengu na kuenea duniani kote. Katika mpango wake, watu weusi wote wangefaa kuangamizwa tu ili watoe nafasi kwa watu aliowaona yeye kuwa bora,

Sasa baada ya sayansi hii ya "kutumbisha" kuvumbuliwa, wataalam wametishika sana.

Wamewaza jinsi ambavyo Hitler angeweza kufanya kama angekuwa mjuzi wa taaluma hiyo.

Kitisho hiki kimezidi kuwatwanga wataalam na wasiokuwa wataalam. Hivi majuzi tu ilipogunduliwa maiti ya msichana wa miaka kumi na minne huko milimarya Andes, Amerika ya

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Kusini. Msichana huyo alikuwa ametolewa kafara miaka karne tano zilizopita lakini hakuoza kwa sababu ya baridi kali ya barafu milimani.

Kwa sababu ya dukuduku la uvumbuzi ambalo haliishi kuutia dhana za kiajabu ubongo wa binadamu. Wataalamu wa "kuchezea" maumbile walipomwona msichana huyo maiti, upesi upesi wakampima. Walipofanya hivyo wakagundua ya kwamba mayai yake ni timamu kabisa wala hayajaharibiwa na mpito wa karne. Papo hapo wengine wakajiwa na wazo la kuyatoa mayai hayo na kuyahifadhi kwenye maabara. Tamaa ikazidi zaidi ya zaidi. Baadhi ya wataalamu wakajiwa na wazo la "kuyaneemesha" mayai hayo na mbegu za uzazi za wanaume. Kwa lengo gani? Kuunda watoto ambao mama yao alikufa zamani za kale ili waonekane watakuwa watu wa aina gani!

Sasa fikiria mwenyewe! Watoto hawa wa maabara wakiwa weledi zaidi ya binadamu yeyote aishiye sasa je? Kwa upande mwingine wakiwa na uwezo mdogo wa kiakili kuliko binadamu yeyote wa kisasa lakini watiifu kama mbwana paka itakuwaje? Hakuna atakayefikiria "kutumbisha" ili tuwe na vijitumwa vyetuu vipenzi majumbani mwetu vinavyofanana nasi badala ya paka na mbwa wasiovishwa nguo?

a) Andika kichwa kifaacho kwa makala haya. . (alamal)

b) Kutumia sayansi ya "kutumbisha" kunaweza kumsaidia binadamu kuangamiza

mabaa gani mawili yanayomkabili sasa? (alamal)

c) Unadhani ni kwa nini wanyama waliozalishwa kwa kutumia sayansi hii bado

wamo maabarani? (alama 3)

d) Fafanua methali "kuchamba kwingi nikuondoka na mavi" kulingana na muktadha

wa habari hii.

e) Kuna ubaya gani kutumbuisha watu? (alama4)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

f) Mwandishi anaonekana kutishwa sana na uwezekano wa sayansi ya kutumbuisha kuishia mikononi mwa "wendawazimu weledi" kwani kuna hatari gani? (alaina 4)

g) Eleza kwa ukamilifu matatizo yanayoweza kuukumba ulimwengu iwapo mayai ya msichana wa Andes yatatumbishwa. (alama 4)

# MATUMIZI YA LUGHA

1. (a) **Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi "O"**
   Mtoto anayelia huchapwa

   (b) **Andika kinyume**

   Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.

   (c) **Andika sentensi tatu ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii:-**
   Kule ndimo alipoingia

   (d) **Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi iuatayo**

   Mama <u>amewahi</u> <u>kupika</u> jikoni

   (e) **Eleza maana ya misemo ifuatayo** :-

   (i) Giza la ukata…
   (ii) Meza mate machungu

   (f) **Unda vitenzi kutokana na :-**

   (i) Mkufunzi
   (ii) Maeneo

   (g) **Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, taja aina za sentensi za kiswahili**

   (h) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale**

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Mwalimu huyu mzuri anafundisha darasani.

(i) **Eleza maana mbili za sentensi :-**

Mama alimlimia mwanawe shamba

(j) **Akifisha sentensi ifuatayo:-**

ah huu ndio upuuzi aliotuitia mmoja wao akaropoka.

(k) **Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano**

(l) **Andika sentensi ifuatayo katika msemo halisi :-**

Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa umetangulia.

(m) **Pambanua viungo vya kisarufi katika kitenzi kifuatacho**

Tuliwalimia

(n) **Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:**

Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (**kanusha kwa umoja**)

(o**) Tunga sentensi ukitumia neno "Vile" kama:**

(i) Kiwakilishi
(ii) Kivumishi
(iii) Kielezi

(p) **Bainisha matumizi viambishi "ku" na "Ji" katika sentensi zifuatazo**:-

(i) Mwanafunzi hukusoma kwa bidii
(ii) Atakupiga
(iii) Amejikata
(iv) Mchezaji huyu ni hodari

(q) **Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha**

Kijibwa changu ni kikali sana

2. (a) **Jaza mapengo**:-

| **Kutenda** | **Kutendesha** |
|---|---|
| (i) Chota | |
| (ii) Lewa | |

(b) **Taja sauti moja ya;**

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(i) King'ong'o
(ii) Kiyeyusho
(c) **Tumia neno "*shujaa*" katika sentensi kama**:-
(i) Kivumishi

(ii) Kielezi...
(d) **Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:-**
Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi
.
(e) **Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa**:-
Kichinjio hiki kilikarabatiwa kwa pesa nyingi

(f) **Eleza maana zinazojitokeza katika vifungu vifuatavyo**:-

(i) Jambazi kutoka dukani liliiba.

(ii) Liliiba jambazi kutoka dukani.
(iii) Kutoka dukani jambazi liliiba.
(iv) Jambazi liliiba kutoka dukani.
(g) **Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi:-**
(i) Vile vitu **ulivyovichanganya** itakubidi

(ii) Bomba hili l**imeziba** mwite fundi aweze

(h) **Unganisha sentensi hii kwa kutumia '*O*' rejeshi :-**
Wavu umekatika. Wavu ni wao

(i) **Eleza matumizi mawili ya "*ka*" na utunge sentensi kwa kila mojawapo**

(j) **Yakinisha sentensi hii**:
Sijafahamu kwa nini hawamkaribishi mpwa wao.

(k) **Andika katika usemi halisi:-**
Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(l) **Akifisha sentensi ifuatayo**:-

Sijaona kitabu kizuri kama mayai waziri wa maradhi, utaniazima siku ngapi bashiri
alimwuliza rita
(m) **Changnanua kwa njia ya mishale**

Mama anapika na baba akisoma gazeti

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(n) **Tunga sentensi moja na uonyeshe kwa mstari**;

(i) Shamirisho kipozi
(ii) Shamirisho kitondo
(iii) Shamirisho ala/kitumizi

(o) **Tungia vitenzi vifuatavyo sentensi katika hali zilizobanwa**:-

(i) Fa(**mazoea**)
(ii) La**(kutendeka**)
(iii) Pa (**kutendea**)

(p) **Tambulisha kishazi tegemezi na kishazi huru**

Wanafunzi walifoanya vyema walituzwa jana

(q) **Pambanua viambishi mbalimbali katika sentensi ifuatayo**

Waliwapendezea

3. a) **Onyesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani:-**

i) Unamjua vyema kweli?

(ii) Hicho wanachokitaka hakipo

(b) **Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi**:-

(i) Minghairi ya

(ii) Wala

(c) **Yakinisha sentensi ifuatayo**:-

Chakula hakipikiki vizuri

(d) **Jibu kulingana na maagizo kwenye mabano:-**

(i) Hatujui ambako alitorokea (**tumia 'O' rejeshi**)

(ii) Angekuwa na pete, angekupatia (**ibadilishe katika wingi kisha uikanishe**)

(e) **Bainisha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo:-**

Maksuudi alimjengea Tamima Kasri kwa matofali mazuri

(f) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale/mistari:-**

Watoto wote wameamka mapema na wazazi wanatayarisha staftahi

(g) **Unda nomino moja moja kwa kila kitenzi**

Shuku
Vumilia
shona
lia

(h) **Eleza maana ya <u>'jinsi'</u> kama inavyojitokeza katika sentensi zifuatazo**

(i) Naomba unionyeshe jinsi ya kuendesha gari
(ii) Wakenya hawapendezwi na jinsi viongozi wanavyoendeleza ufisadi

(i) **Bainisha aina za nomino zilizopigiwa mistari katika sentensi hii:-**
**<u>Uhodari</u>** wa **<u>wanariadha</u>** wa **<u>Kenya</u>** unahitajika kote duniani

(j) **Tunga sentensi ukitumia mzizi – choyo kama** :-
(i) nomino

(ii) Kivumishi

(iii) Kiwakilishi

(k) **Eleza matumizi <u>mawili</u> ya kila mojawapo wa alama za uakifishaji zifuatazo**:-
(i) msitari

(ii) Parandesi

(l) **Geuza zentensi zifuatazo katika kauli kwenye mabano**:-
(i) Fundi ameharibu saa (**kutendea)**

(ii) Umemwona mgeni? (**kutendewa**)

(m) **Andika kwa udogo:-**
Gari la Mzee Maritu limegonga ng'ombe wa jirani wake

## 4.MATUMIZI YA LUGHA

(a) Andika sentensi ifuatayo bila kutumia "amba"
(i) Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali. *(alama 1)*
(ii) Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea. *(alama 2)*

(b) Badilisha sentensi hizi hadi usemi wa taarifa
(i) "Nitarudi tu ikiwa mtakubali kuomba msamaha." Juma alisema. *(alama 2)*

(ii) "Elezeni vile mlivyokuja hapa na namna mtakavyokwenda." Mwalimu mkuu alisema *(alama 3)*

(c) Fuata maagizo uliyopewa baada ya kila sentensi ili kujibu maswali haya.

(i) Aliogopa kumwangalia simba aliyekula mzoga. (Tumia neno 'Ogofya' bila ya kubadilisha maana ya sentensi) *(alama 2)*

(ii) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ukiwa unatumia msumeno. (Anza Ni rahisi . . .) *(alama 2)*

d) (i) Eleza maana na matumizi ya methali hii *(alama 2)*
Kila mchukuzi husifu mzigo wake

(ii) Kamilisha tashbihi hizi *(alama 2)*
...............kama mauti
Nuka kama..............

(e) (i) Kanusha sentensi hii *(alama 2)*
Tungewalaki kama tungejua watakuja

(ii) Sahihisha sentensi ifuatayo na uiweke katika wingi *(alama 2)*
Ningalifanya kazi ningekuwa tajiri

(f) Tunga sentensi nne kuonyesha matumizi na maana nne za kijineno ki

(g) Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi *(alama 4)*

(i) Bibi yule alinunua gari ________________ (-pya)
(ii) Mwizi alifukuzwa na mbwa ________________ (-angu)
(iii) Mti (-ingine) __________________ uliangushwa badala ya ule wa kwanza.
(iv) Nyoka aliingia _______________ (-le) shimoni.

(h) Unda majina mawili kutoka vitenzi hivi na utumie katika sentensi ili kubainisha maana *(alama 4)*

(i) Safiri
(ii) Zaa

(i) Akifisha kifungu hiki
Yohana na emanueli walifunga safari wakielekea mashariki kusini na hatimaye magharibi walifika huko novemba mwaka jana walipokuwa wakirudi walimkuta mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale *(alama 4)*

(j) (i) Geuza sentensi hii hadi udogo *(alama 2)*
Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi.

(ii) Eleza umuhimu wa sehemu hizi za mwili
* Figo
* Moyo

## 5. MATUMIZI YA LUGHA.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

a) Tumia kiulizi - pi katika kujaza sehemu zilizoachwa wazi. ***( alama 4 )***

i) Ni tunda ____________ ulilolеta ?
ii) Ni mayai ___________ yaliyovunjwa ?
iii) Ni kiwete __________ aliyepata msaada ?
iv) Ni mitume __________ waliojilolea kufanya kazi ?

**b) Andika sentensi zifuatazo katika kauli ya kufanyisha / za** ***( alama 4 )***

i) Alikifanya kijiti kiingie ndani ya kufuli.
ii) Mzazi alimfanya mwanawe alime siku nzima

**c) Tumia virejeleo vifavyo katika sentensi hizi.**

i) Mchezaji alipiga mpira kwa ustadi
ii) Simba alifukuza mtalii aliyetaka kupiga picha
iii) Umeokota wapi ndizi hizi zote ?
iv) Andrea alipanga vizuri maua mezani

**d) Andika tena sentensi hizi ili zisiwe katika hali ya kukanusha** ***( alama 4 )***

i) Asiyekujua hakuthamini
ii) Asiyejua maana haambiwi maana
iii) Fimbo ya mbali haiui nyoka
iv) Amani haiji ila kwa ncha ya upanga

**e) Ziandike sentensi hizi kwa kufuata maagizo**

i) Mlete mtu mwenye akili ( tumia 'amba' )
ii) Walifungana bao moja kwa moja katika mchezo ule ( tumia …… Sare )

**f) Unda majina kutoka vitenzi hivi** ( alama 2 )

i) Kulia __________________________ , Kudhani _______________________
ii) Ni nini maana ya : Amepata ahueni (alama 1 )
Amekuwa buge ( alama 1 )

**g) Andika sentensi ifuatayo katika udogo** **( alama 2 )**

i) Alishikwa na jipu ambalo lilivimbisha dole lake la mguu mithili ya pesa
ii) Akifisha sentensi hii: ( Alama 2 )
Ondiek aliita Maria Maria njoo hapa.

**h) Eleza matumizi ya 'Ki' katika sentensi hizi:**

i) Nitakapokuwa ni<u>ki</u>lala atakuwa a<u>ki</u>durusu
ii) <u>Ki</u>vulana hicho <u>ki</u>nawafurahisha wenzake

**i) Andika maana mbili zinazojitokeza katika kila moja ya sentensi hizi**

i) Mwalimu alimsomea mwanafunzi
ii) Alimlilia mwanawe

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP**
**0705525657/0770195807**

j) Ikiwa Mtondo ni Jumamosi

i.) Juzi ni siku gani ______________________________ (alama 1)

ii) Leo ni siku gani ______________________________ ( alama 1)

iii) Tunga sentensi mbili ukutumia tashbihi zinazotokana na maneno haya: ( baidika, mkizi) ( alama10 )

## 6.MATUMIZI YA LUGHA.

(a) Andika sentensi hizi kwa wingi (alama 4)

(i) Buzi lililoibwa na jambazi lile limepatikana

(ii) Mwenye kelele usidhani kapoa

(b) Tunga sentensi ukitumia tashbihi zinazotokana na maneno yafuatayo

(i) Gundi

(ii) Chiriku

(iii) Lumbwi

(iv) Wali wa daku

(c) Kuna tofauti gani kati ya vyombo hivi

(i) Dira / saa

(ii) Tofautisha maneno haya

(iii) Sulubu / suluhu

(d) Sahihisha sentensi hizi (alama 4)

(i) Munyi alisanya vitabu yote siku ya Ijumaa

(ii) Fupa huu ulivunjwa na mpwakoko hii

(e) Andika sentensi ifuatayo bila kutumia neno 'amba'

(i) Jembe ambalo lilinunuliwa jana limevunjika mpini (alama 2)

(iii) Mwizi ambaye amekuwa akitusumbua ameshikwa

(alama 2)

(f) Fuata maagizo uliyopewa katika kujibu yafuatayo

(i) Soma kwa bidii kijana. Utafaulu katika mitihani yako. (tumia …… nge) (alama 2)

(ii) Kisu kinachonolewa ndicho kinachopata (geuza hadi hali ya mazoea) (alama 2)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(g) Andika maneno mengine mawili yenye maana sawa na yafuatayo (alama 4)

(i) Daawa
(ii) Bughudha
(iv) Abadani
(v) Fitina

(h) Kanusha sentensi hizi

(i) Mwana yule alikuwa amekamilisha kuchimba mtaro alipojikata mguu
(ii) King'ora kililia kioo kilipovunjwa

(i) Weka viambisho vinavyofaa sentensi zifuatazo

(i) Walimu ______ li ____ ona mtoto _______ dogo ________ kianguka matopeni.
(i) Mwavuli huu __________ eusi __________ a mzungu ame _____________ nunua jana.

(j) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kufanyiza

(i) Mwalimu amefanya mwanafunzi wake ajue umuhimu wa bidii masomoni

(alama 2)

(ii) Paka ameyanywa maziwa (geuza hadi kauli ya kufanywa) (alama 2)

# ISIMUJAMII

1.

| | |
|---|---|
| Saidi | : Hallo............Hallo....Huyo ni Bw. Mohamed? |
| Mohamed | : Ndio...uko wapi... |
| Saidi | : Shuleni...sasa...ulinifikishia ujumbe? |
| Mohamed | : La. Parade ilikuwa imehitimishwa |
| Saidi | : Sina credit. Nipigie tafadhali. |
| Mohamed | : Sina pia, nitatuma sms |
| Saidi | : Iwe saa hii eh? |
| Mohamed | : Baada ya dakika tano |
| Saidi | : Good day |
| Mohamed | : Welcome |

(a) Taja na uthibitishe sifa zinazojitokeza katika mazungumzo haya

(b) Eleza sababu za wazungumzaji kutumiambinu zifuatazo katika mazungumzo yao

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(i) Mdokezo

(ii) Lugha mseto

2. Lugha ya kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Yataje na kuyaeleza.

3. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***

Uchunguzi uliofanywa umeonyesha kuwa anasumbuliwa na uto mwingi mwilini. Uto unaweza kudondoshwa kwa kufanya mazoezi, kupunguza ulaji wa vyakula vya wanga na hata protini. Protini iwapo nyingi mwilini hugeuzwa kuwa glukosi ambayo huhifadhiwa mwilini. Hii huwa msingi wa unene pia ambao unahatarisha afya. Jamaa yake aliyeaga dunia alikuwa mgonjwa wa bolisukari ambayo inaweza kurithishwa. Kimsingi, lazima awe na welewa bora kabisa wa lishe. Mwenzake naye aliathiriwa na **aflatoxins** zilikuwa kwenye chakula alichokula.

(a) Sajili hii inapatikana wapi? Kwa nini?

(b) Taja sifa zinazohusishwa na sajili yenyewe

# USHAIRI

**1. SHAIRI 'A'.**

Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
Watoto Wakukimbia

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza Panya
Akalia kulikuwa na pala
Kichwani
Mchawi kutaka sana kutisha

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Alijigeuza Simba
Akalia na risasi kichwani

Jongoo kutaka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa yatakwenda
Bwanako kumpa sumu ?
Hadija umeshika nyoka kwa mkia
Hadija umepitia nyuma ya punda

**SHAIRI 'B'**

Piteni jamani, Piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka

Vijana kwa nini hampiti ?
Kwa nini mwanicheka kisogo ?
Mzigo niliobeba haupo.

Lakini umenipinda ngongo na
Nendako
Haya piteni ! Piteni haraka ! Heei !

Mwafikiri mwaniacha nyuma !
Njia ya maisha ni moja tu.
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengi wenu
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kutazama
Ningewambia siti miaka
Mingi.

(a) Haya ni mashairi ya aina gani ? Toa saabu
(b) Washairi hawa wawili wanalalamika. Yafafanue malalamishi yao
(c) Onyesha jinsi kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(d) Ni vipi Hadija :-
(i) Amekata mti mtima ?
(ii) Amepita nyuma ya Punda
(al.2)
(e) Toa mifano 2 ya uhuru wa mashairi kwa kurejelea mashairi haya
(f) Kwa kurejelea shairi '**B**' eleza maana ya:-
(i) Mzigo
(ii) Siri
(iii) Kula nimekula
(iv) Niko nyuma ya wakati

2. Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwandani.
Afya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini
Sisi tokea **azali**, twende zetu mizumuni
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu za kirijali, Mkuyati uamini
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani
Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zongo huanoni
Zabadili pia **sahali,** kwa maradhi yalo ndani
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini
Daktari k'ona mwili, tanena kensa tumboni
Visu visitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama fagili, **tumbo nyangwe** na maini
Nifuateni sipitalini, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi **dhalili**, kutenguliwa tegoni
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Wambiwa damu kaliti, ndugu msaidieni
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, Wakueleze undani.
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu thamani

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP**
**0705525657/0770195807**

Utete huku wawili, wa manjano na kijani
Matunda pia asali, vitu vyae shamoni
Nifuateni sipati, na dawa zi langoni?

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka

(b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili

(c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitalini

(d) Eleza umbo la shairi hili
(al. 6

(e) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi ?

(f) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye shairi :-

(i) Dhalili –
..........................................................................................................................

(ii) Azali -
..........................................................................................................................

(iii) Sahali -
..........................................................................................................................

(iv) Tumbo nyanywe
..........................................................................................................

3. **WAFULA KABILIANA NA KISU**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamme,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu !
Iwapo utatingiza kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu,
Ndege zote ziangamie.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,

Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa,
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri

**<u>Maswali</u>**

(a) Hili ni shairi la aina gani ? Thibitisha

(b) Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ?

(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume

(d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili

(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili

(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili

(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili ?

(i) Mbari

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Msununu
(iii) Ngariba
(iv) Uvundo

4. **HATIMA YANGU**

1. Mke wangu wameshanipoka
Ndugu zangu, wamedai ububu
Wazazi kuzoea kunigombeza

2. Juzi mali lilimbikiza
Furaha lilitanda
Makanwa yalijaziwa
Hoi hoi ikawa desturi

3. Kilabu tulikwenda
Nyama tulichoma
Mahali tulizuru
Tuliteremsha!

4. Leo mambo yamenigeuka
Wao masahibu siwaoni
Matumbo yakaninguruma
Kama radi ya mvua

5. Nyumbani nimebaki pweke
Mke amenitoroka
Watoto wameparara
Skuli kugharamia
Imegeuka balaa belua

6. Ndipo nimeamua
Afadhali kitanzi badala ya balaa
Kumbe kupanga ndiyo maana
Maisha na waasia

(a) Eleza mambo muhimu yanayoelezwa katika shairi hili

(b) Fafanua sifa mbili za anayezungumza katika shairi

(c) Dondoa na ufafanue mbinu zozote mbili za lugha katika shairi hili

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP**
**0705525657/0770195807**

(d) Eleza maana ya:-

(i) Ndugu zangu wamedai ububu

(ii) Kumbe kupanga ndiyo maana

5. **Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali**

Cheo cha mtu hupanda, ukipata mke mwema,
Kula chachu na maganda, mfano kama mnyama,
Na nyumba iwe kibanda, si nzuri ya kutazama,
Utaona umewanda, moyo umekuterema.

Mke mwema ni johari, yenye furaha daima,
Awe hasa na saburi, na adili na huruma,
Hata ukiwa fakiri, hutimizi pato jema,
Utaona tajiri, maliki dunia nzima.

Mke akiwa mbishi, wa kushindana kusema,
Na majivuno na mashi, na ulimi wake pima,
Hata kama wala pishi, wali na kilo ya nyama,
Utajiona waishi, duniani huna kima.

Mke mrembo si hoja, hili nimekwisha pima,
Nimepima rejareja, kila jambo kutazama,
Kujumlisha pamoja, mambo yalivyosimama,
Nikaona kuwa tija, ndogo kuliko gharama.

Awe mwema mke wangu, nani hapendi kusema?
Wema asili ya ungu, milele una heshima,
Kuwa wema walimwengu, ni wajibu na lazima,
Wema dawa ya machungu, moyoni yanayouma.

**<u>Maswali</u>**

(a) Kulingana na shairi hili, mke mwema ana faida gani kwa mumewe? *(alama 3)*
(b) Mke mwema ana sifa gani? *(alama 3)*
(c) Mwandishi wa shairi hili alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili? *(alama 3)*
(d) Eleza kwa ufupi muundo wa shairi hili. *(alama 6)*
(e) Maneno yafuatayo yametumiwa katika shairi kuleta maana gani? *(alama 5)*
- (i) Chachu
- (ii) Johari
- (iii) Saburi
- (iv) Mbishi
- (i) Pishi

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

6. Nataka nikupe chanzo, weka katika moyo,
Kishike kwa mkazo, hata kizae mazao,
Ukifanya bidiizo, kushawishi utakayo,
Utaona mfulizo, kwako yanakuja mbio

Husemwa Alexander, shujaa Macedonia,
Ambaye alishinda, karibu nzima dunia,
Alipokosa pa kwenda, tena kushambulia,
Kwa huzuni alikonda, akadiriki kulia,

Ingawa vita vigumu, yeye alivipenda,
Kwa moyo aliazimu, daima mbele kwenda,
Moyo kuitia hamu, mashaka kuyashinda,
Ndilo linalolazimu, kila mtu kutenda.

Moyo ukiulegeza, kila kitu kigumu,
Utaishi na kuoza, hupati kuonja tamu,
Lakini ukijikaza, ipasavyo mwanadamu,
Katika mwangaza, utakuwa na sehemu.

Moyo kuupa mwanzo, wa kushindwa hustawi,
Utaona mzozo, unalotaka haliwi,
Na hili ni katizo, ya faida ya uhai,
Peponi halina tuzo, na hapa ni uadui

Hili linahasiri, moyoni kulidhibiti,
Mabaya ukifikiri, yaliyo mema hupati,
Na kila wazo la heri, hukaribisha bahati,
Fikira iliyo nzuri, sawasawa na yakuti.

**Maswali**

(a) Kilichomfanya Alexander kufaulu katika kadhia zake ni nini hasa? *(alama 3)*
(b) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. *(alama 4)*
(c) Kuna athari gani kwa kukosa moyo wa ujasiri? *(alama 3)*
(d) Mtunzi huyu ana dosari gani kwa upande wa muundo wa shairi? *(alama 4)*
(e) ‘Kwa huzuni alikonda, akadiriki kulia.’ Ni kwa nini ilitukia hivi? *(alama 3)*
(f) Eleza maana ya maneno haya. *(alama 3)*
  (i) Akadiriki
  (ii) Kushawishi
  (iii) Kulidhibiti

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

7. Mabadiliko lazima kwa watu ulimwenguni,
Nalo lilianza zama hakika si neno geni,
Ni tabia ya daima kipya kuwa cha zamani,
Kwa watu ulimwenguni mabadiliko lazima.

Kama hili halikuwa jipya lingekuja lini ?
Mfano wetu maua na majani mitini
Hili linapofumua, lile huanguka chini
Jipya lingekuja lini kama hili halikuwa

Kuwapo na kutowapo tumo mabadilikoni
Nakuapia kiapo kwamba hii ni kanuni
Nawe linganisha pepo kaskazi na kusini
Tumo mabadilikoni kuwapo na kutowapo

Tukitaka tusitake ni sheria tumo ndani
Waume na wanawake roho zote za manani
Kubadili mwendo wake dunia si yamkini
Ni sheria tumo ndani tukitaka tusitake

Mwendo wa dunia mbio haimo usingizini
Kwa aliye na kilio na aliye furahani
Mara huona machweo na mara jua kichwani
Haimo usingizini mwendo wa dunia mbio

Mbio maisha ya watu, mfululizo mbioni
Hali hii kila kitu, kilicho maumbileni
Mbio haingoji mtu – tuo haijulikani
Mfululizo mbioni, mbio maisha ya watu

Hutuchukua kwa zamu katika matumaini
Na mchungu na matamu hututokea njiani
Na mara hatufahamu lilikuwa jambo gani
Katika matumaini hutuchukua kwa zamu.

***Maswali.***

a) Kuna mifano mingi ya kimaumbile iliyotolewa ili kudhihirisha dhana hii ya mabadiliko. Itaje mifano yoyote mitatu. ( alama 3 )
b) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari ( alama 4 )
c) Kuna ithibati kuwa mabadiliko hayabagui ? ( alama 4)
d) Nakili mishororo minne inayoeleza kuwa mabadiliko ni sharti maishani ( alama 4 )
e) Katika shairi hili mwandishi ametaja maneno na vinyume vyao. Toa majozi manne ya maneno haya ( neno na kinyume chake ) ( alama 2 )

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

i) Linapofumua
ii) Kiapo
iii) Tuo ( alama 3 )

8. Tusitake kusimama, bila kwanza kutambaa,
Au dede kuwa hima, kabula hatuyakaa
Tutakapo kuchutama, kuinama kunafaa
Tujihimu kujinyima, makubwa kutoyauyaa

Tusitake kuenenda, guli lisipokomaa
Tujizonge na mikanda, inapochagiza njaa
Na mazuri tukipenda, ni lazima kuyaandaa
Tujiase kujipinda, kujepusha na balaa
Tusitake uvulana, au siga kuzagaa
Tushikaye nyonga sana, tunuiyapo kupaa
Kama uwezo hapana, tutoelee dagaa
Tujiase hicho kina, maji yajapokujaa

Tusitake vya wenzetu, walochuma kwa hadaa
Wanaofyatua vitu, na kisha vikasambaa
Uwezo hatuna katu, umaskini fazaa
Tujihimu kula vyetu, siendekeze tamaa

Mtaka kuiga watu, kufata kubwa rubaa
Vyao vijaile kwetu, vifaa vingi vifaa
Tunamezwa na machatu, tusibakishwe dhiraa
Tujihimu kilo chetu, hata kama twapagaa

## Maswali

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)
(b) Chambua ubeti wa tatu na nne kwa upande wa vina na mizani (alama 4)
(c) Thibitihsha jinsi kunga ya inkisari na mazida inayojitokeza katika shairi hili

(alama 3)

(d) Mwandishi ana ujumbe gani katika shairi hili kwa wasomaji wake? (alama 2)
(e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari (alama 4)
(f) Taja misamiati yoyote minne ya hatua ya maisha ya binadamu na ueleze yake.
(alama 4)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

9. Alikuwa mtu duni, alozongwa na shakawa
Hana alichoauni, wala alichoambuwa
Walikimwita mhuni, na thamani kumtewa
Utamwonea amani, jinsi ya alivyokuwa
Mwepesi wa kusahau

Alipita mtaani, kuomba kusaidiwa
Mtoto wa kimaskini, riziki haizumbuwa
Alizubaa njini, lake jua na mvuwa
Mwepesi wa kusahau

Ekosa kwenda chuoni, kwani alibaguliwa
Daima kawa mbooni, akitafuta afuwa
Chumia chungu mekoni, furaha kwake haiwa
Mwepesi wa kusahau

Wakati ukabaini, mjiuga akatambuwa
'Katoka usingizini, napo kwenye kukawa
Watu wakamuamini, kuwa mtu wa mvuwa
Kumbe vile atahuni, na ujeuri kuingiwa
Mwepesi wa kusahau

Leo kawa Sultani, mwingine katu hajawa
Hatamani na haoni, nyuma aliyochukuwa
Anga kwake limeguni, gubi amegubiliwa
Mwanadamu maalum, hakika ukichinguwa
Mwepesi wa kusahau

## Maswali

(a) Eleza ujumbe unayojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili (alama 4)
(b) Fafanua maana ya kibwagizo katika shairi hili (alama 3)
(c) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu (alama 2)
(d) Je mwandishi amefaulu katika kuzingatia arudhi za utunzi? Fafanua (alama 6)
(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 5)
- (i) Alichoauni
- (ii) Alizubaa
- (iii) Ukabaini
- (iv) Sultani
- (v) Maluum

**10. Soma shairi lifuatalo kwa makini halafu ujibu maswali yanayofuata**

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

1. Naja sasa ni ndiyani, naja kwetu <u>Mzalendo</u>
Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando
Kwetu' mi nakutamani, kulo na mwingi uhondo
Nijaye ni yule nyundo, misumari hadharini

2. Naja kwingine kuwapi, kulojaa langu pendo?
Huenda nende kwinginepi, sawa nako kwa muundo?
Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando?
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

3. Naja nije rudi papo, panigedeme mgando
Ningaambwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo
Sitakwenda penginepo, tarudi kuko kwa <u>mwando</u>
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

4. Naja sitapakimbiya, <u>ningambwa</u> kuna vimondo
'Takuja kuvilekeya, vinganijiya kwa vundo
nilipozawa tafiya, sikimbii kwenda kando
nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

5. Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivyo mwando
Tena n'najiandaa, kwa fikira na vitendo
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

6. Naja na ingawa naja, siwaeki mifundo
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendwa mwando
Ela wataoningoja, na vyao viwi vitendo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

7. a) Eleza jinsi 'uzalendo' wa mshairi unavyojitokeza katika beti za 1 na 2 alama 4

b) Fafanua jazanda zinazopatikana katika mshororo:

Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando? alama 2

c) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari alama 4

d) (i) Katika ubeti wa 5 mshairi amebadilika Eleza alama 2

(ii) Ananuia kufanya nini pindi arudipo? Alama 2

e) Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa 6 alama 2

f) Andika maneno haya katika kiswahili sanifu alama 2

a. Mwando
b. Ningambwa

g) Kibwagizo cha shairi kinampa sifa gani mshairi? Alama 2

**11.Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Jukwani naingia, huku hapa pasokota,
Kwa uchungu ninalia,hii tumbo nitaikata,
Msiba mejiletea,nimekila kiso takata,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Wazee hata vijana,wote umewasubua,

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Huruma nao hauna,heshima kawakosea,
Ukambani na Sagana,hata mbwa wararua,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Wahasibu ofisini,kibwebwe mejifunga,
Miaka mingi vitabuni,ili wasikose unga,
Nadhari wanadhamini,hesabu wanazirenga,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wapenzi wa kiholela,pia wanakuogopa,
Baada yao kulala, wana wao wanatupa,
Wakihitaji chakula,wanachokora mapipa,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Wafugaji hata nao,kama dawa wakwamini,
Hawajali jiranio,wamesusia amani,
Wanaiba ng'ombe wao,na kuzua kisirani,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Nayo mizozo ya maji, kaonekana kwa mara,
Hiyo nayo ni dibaji,sababu sio harara,
Njaa wahepe wenyeji, huo ndio mkarara,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

Ningeweza kukuuza,ingekuwa siku njema,
Tena kwa bei ya meza,sokoni nimesimama,
Wala tena singewaza,kuhusu wali na sima,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Hatima umefikika,naenda zangu nikale,
Mate yanidondoka,kwa mnukio wa wale,
Naomba kwenda kukaa,wala sio nikalale,
We tumbo nitakupani,uwe umetosheka?

## Maswali

i Lipe anwani mwafaka shairi hili. (Alama 2)

ii Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (Alama 2)

iii Huku ukitolea mifano mwafaka, taja arudhi zilizotumiwa katika ubeti wa tatu. (Alama 4)

iv Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (Alama 4)

v Thibitisha kuwepo kwa idhini ya ushairi. (Alama 2)

vi Taja madhila anayoelezea mtunzi wa shairi hili yaletwayo na tumbo. (Alama 4)

vii Elezea maana ya maneno yafuatayo. (Alama 2)

(a) Dibaji

(b) Harara

## 12. **LAU HAKUNA MAUTI. Na Abdalla Said Kizere**

1. Lau dunia nanena, tuseme si ati ati,
Mauti kawa hakuna, katika wote wakati,
Vipi tungelisongana, tunaoishi tiati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

2. Dunia ingetatana, na kizazi katikati,
Huku kwazaliwa bwana, kule kwazawa binti,
Vipi tungelioana, na kuzaa hatuwati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

3. Lau mauti hakuna, tungesongana sharuti,
Kwa viumbe kukazana, wanadamu na manyati,
Vipi tungelijazana, kwa kusitawi umati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

4. Walakini Subuhana, kapanga sisi na miti,
Ili tusizidi sana, si wengi na si katiti
Maisha ya kupishana, yule ende yule keti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

5. Ndipo dunia kufana, ikawa kama yakuti,
Kwa uwezowe Rabana, kaipanga madhubuti,
Maisha kugawiana, kayagawa kwa mauti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

6. Njia ingekuwa hapana, pembeni na katikati,
Sote tungeambatana, kama ukosi na shati,
Na njaa ingetutafuna, pa kulima hatupati,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

7. Peleleza utaona, hayataki utafiti,
Kama tungelikongana, ingekuwa ni bahati,
Vipi tungesukumana, katika hiyo hayati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

8. Mbele sitokwenda tena, hapa mwisho nasukuti,
Yaoleni waungwana, shauri yake Jabaruti,
Yote tuloelezana, katenda bila senti,

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

**MASWALI**

a) Je, hili ni shairi la bahari gani? Eleza (alama 2)

b) Eleza vile mwandishi alivyotumia uhuru wa kishairi (alama 4)

c) Eleza umbo la shairi hili (alama 4)

d) Fafanua ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano (alama 4)

e) Andika majina mawili ya Mungu kwa mujibu wa shairi (alama 2)

f) Kwa kutolea mifano, eleza mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na shairi (alama 2)

(i) Tiati __________________

(ii) Shani__________________

**13. Soma shairi lifuatalo, kisha ujibu maswali; (alama 20)**

Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwendani,
Afiya yangu dhahili, mno nataka amani,
Nawe umenikabili, nenende sipitalini,
Sisi tokea azali, twenda zetu mizimuni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani,
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini,

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Kwa nguvu za kirijali, mkuyati uamini,
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele Fulani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zongo huauni,
Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalondani,
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini,
Dakitari k'ona mwili, tanena kensa tumboni,
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni,
Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani,
Wambiwa damu kalili, ndugu msaidieni,
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo buriani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu thamani,
Ulete kuku wawili, wa manjano na kijani,
Matunda pia asali, vitu vyae chanoni,
Nafwatani sipitali, na dawa zi mlangoni?

**MASWALI – USHAIRI**

**(ALAMA 20)**

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)

b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili? (alama 2)

c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitali? (alama 4)

d) Kwa kuzingatia muundo wa shairi hili, eleza mbinu zilizotumika (alama 6)

e) kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi? (alama 2)

f) **Andika maana ya maneno yafuatayo yalivyotumika katika shairi** (alama 4)

i) Dhahili

ii) Azali

iii) Sahali

iv) Tumbo nyangwe

**14. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali.**

Niokoa Muokozi, uniondolee mashaka.
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekithiri simanzi, ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo.

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua
Naomba hisikitika, na mikono hiinua
Mtenda ndiwe Moliwa, nipate niyatakayo.

Mtenda ndiwe Moliwa, we ndiwe Mola wa anga
Mazito kuyaondoa, pamoja na kuyatenga

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilonifunga
Nikundulia muwanga, nipate niyatakayo

Muwanga nikundulia, nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea, itoke mwangu moyoni
Mambo mema niegheshea, maovu nisitamani.
Nitendea we Manani, nipate niyatakayo.

Igeuze yangu nia, dhaifu unipe mema
Nili katika dunia, kwa afia na uzima
Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema
Nifurahike mtima, nipate niyatakayo.

(a) Shairi hili ni la bahari gani? Eleza. (alama 2)

(b) Taja madhumuni ya shairi hili. (alama 3)

(c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

(d) Thibitisha namna uhuru wa kishairi unaibuka katika shairi. (alama 4)

(e) Andika ubeti wa pili katika lugha sufufu. (alama 4)

(f) Toa maana ya:

(i) Nimedhikika

(ii) Muwanga nikundulia

(iii) Nifurahike mtima (alama 3)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

# FASIHI SIMULIZI

1. ***Soma kisha ujibu maswali***

Lala mtoto lala x2
Mama atakuja lala
Alienda sokoni lala
Aje na ndizi  lala
Ndizi ya mtoto lala
Na maziwa ya mtoto lala
Andazi lako akirudi
Pia nyama ya kifupa
Kifupa, kwangu, wewe kinofu
Kipenzi mwana lala x2

Titi laja x2

Basi kipenzi lala
Baba atakuja lala
Aje na mkate lala
Mkate wa mtoto lala
Tanona ja ndovu lala

**<u>Maswali</u>**

(a) Huku ukithibitisha jibu lako eleza huu ni wimbo wa aina gani?

(b) Eleza sifa za wimbo wa aina hii

(c) Onyesha umuhimu wa wimbo huu

(d) Eleza amali kuhusu jamii zinazojitokeza katika wimbo huu

(e) Tambua mbinu zozote **mbili** za utunzi zilizotumika katika wimbo huu

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(f) Taja vitendo **viwili** vinavyoambatana na uimbaji wa aina hii ya wimbo

(g) Wimbo huu una wahusika wangapi? Wataje

2. ***Soma hadithi hii halafu ujibu maswali ulivyoulizwa***

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme "wanadamu hamtakufa." Kinyonga alienda kwa mwendo wa kuduwaa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akaseme, "Mwanadamu sharti kufa." Mjusi aliunyanyua mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, "Wanadamu sharti kufa!" Akarejelea haraka kwa Mungu. Baada ya muda kinyonga naye akafika duniana na kutangaza, "Wanadamu hamtakufa!" Wanadamu wakapinga mara na kusema, "La! Tumeshapata ujumbe wa Mjusi, wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la mjusi, wanadamu hufa.

**<u>Maswali</u>**

(a) (i) Hadithi hii huitwaje?

(ii) Toa sababu zako

(b) Eleza **sifa tatu** zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii

(c) Kinyonga ni mhusika wa aina gani?

(d) Hadithi hii ina umuhimu gani?

(e) Taja njia zozote **nne** za kukusanya kazi za fasihi simulizi

(f) **Tambulisha vipera hivi**:-

(i) Kula hepi
(ii) Sema yako ni ya kuazima
(iii) Baba wa Taifa

3. (a) Fafanua sifa **tatu** za ushairi simulizi

(b) Wawe na kimai ni nini katika fasihi simulizi? Eleza faida zake

(c) Ainisha mambo yanayobainisha muundo wa nyimbo

(d) Jadili muundo wa kitendawili

(e) Bainisha tamathali za usemi zilizotumika katika methali zifuatazo:-
(i) Ujana ni moshi ukienda haurudi

(ii) Usipoziba ufaa utajenga ukuta

(f) Jadili kwa kina matatizo ambayo huenda yakakabili fasihi simulizi katika jamii ya kesho
kisha utoe mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na hali hii

# MSAMIATI

**1.**

(a) I *Zifuatazo ni sehemu gani za mwili*

(i) Kisugudi

(ii) Nguyu

II *Andika maneno mengine yenye* maana sawa na

i) Damu , ii) Jura

(b) *Tumia kitenzi **<u>KAA</u>** inavyofaa kujaza nafasvzilizoachwa*

Onyango alipofika nyumbani alikosa mahali pa..............

Watu walikuwa wamejaa na hapakuwa na kitihata kimpja cha. (alama 2)

(c) *Fafanna maana ya methali*

I Wasohayawariamjiwao

II Tunasema kifurushi cha kalamu

............................... ya ndizi

(d) Ni *mbinu gani za lugha zinzotumiwa katika sentensi hizi?*

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP**
**0705525657/0770195807**

I Juma si simba wetu hapa kijijini

II Jymanishujaakama samba

(e) *Andika sentensi tatu kuonyesha maana tatu tofauti za neno* KINA (alama 3)

(f) *Eleza tofauti ya semi mbili zilizopigwa mstari*

i) Kevogo <u>hana muhali</u>; ikiwa hawezi kukufanyia iambo atakwambia

ii) Kevogo <u>hana muhali</u>; hivi sasa amekuambia hawezi kukufanvia janabo hil

g) *Yaandike maneno yajuatayo katika ufupi wake*

(i) Shangazizako

(ii) Mama zako

3.

(a) *Fafanna maana za misemo ifuatayo kwa kuitungia sentensi*

(i) Kula uvundo

(ii) kulauhondo (alama2)

(iii) kula mori

(b) *Eleza kazi ifanywayo na:*

(i) Mhariri

(ii) Jasusi

**3.**

(a) i) Eleza *maana ya misemo ifuatayo kwa kuitungia sentensi moja moja*

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Kuramba kisogo (alama2)

Kuzunguka mbuyu (alama2)

ii) *Andika methali nyingine ambayo maanayake ni kinyume cha*

Riziki kama ajali huitambui ijapo

Mahali palipo hamwa panaitwa (alamal)

4.

(a) Taja madini mawili ambayo yametukuzwa zaidi, moja kwa tharnani yake ya kifedha na nyingine kwa kutengeneza vyuma vigumu kuliko madini mengine

(alama 2) (b) *Watu wafuatao wanafanya kazi gani* (alama 2)

(i) Mhasibu.........................................................................................

(ii) Mhazili.........................................................................................

(c) Eleza *tofauti mbili muhimu za kimaumbile kat ya wanyama*

(i) Kifaru

(ii) Nyati (alama 4) (d)

*Tumia semi hizi katika sentensi kuonyesha maana:*

(i) Kuchokoachokoa maneno (alama 2)

(ii) kumeza shubiri (alama2)

(e) *Tunga sentensi mbili zinazobainisha tofauti kati ya*

(i) Goma

Koma (alama2)

**5.**

(a) (i) *Andika metbali nyinging yenye maana na:*

Mweriye kelele hana neon (alama 1)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) *Eleza maana yamisemo*

I. Hanamwiko........................................................................

II. Ameliambugimiguuni..................................................................
..

(alama 2)

(b) *Tunga sentensi mbili kuonyesha tofauti kati ya*

(i) Tega

(ii) Tenga (alama 2)

(c) *Eleza maana mbili mbili tofauti za maneno:*

(i) Rudi

(ii) Funza

d) jumba la kuhifadhi vitu vya kale ili watu wavitazarm huitwa

(e) A*ndika kwa tarakimu:*

Nusu kuonueza sudusi ni sawabn na thuluthi mbili

(f) Jaza kiungo cha niwili ki faacho:

(i) _ _ ya jicho hurekebisha kiasi cha mwanga uingiao kwenye jicho

(alama 1)

(ii) (alama 1}

Saa hukmgiwa kwenye ____ cha mkono

(g) (i)

Mjukuu ni wo habu; mpwa ni wa (aiama 1)

(alama 1}

6. *Tunawaitaje watu hawa* (*alama* 2)

i) Mtu anayebeba mzigo kwa ujira (ii) Mtu anayeshugliulikia elimu ya nyota

(b) *Taja methali inayoafikiana na maelezo haya:*

i) Wengine wanapozozanana kugombana, kunao wanaoiiirahia kabisa hali hiya

ii) Afadhali kuhudhuria huo mkutano hata kama umechelewa

(c) *Tunga sentensi tatu zikionyesha maana tatu za neno <u>chungu</u>* (alama 1)

(d) ***Kamilisha***

i)

Bumba

la, ii)

Genge

la

(e) (i) Juhudi zake hizo si chochote bali kutapatapa kwa mfamaji

(ii) Leo kapasua yote, hata mtama kwarnwagia kuku

(ii) Tunachunga unga. tunapeta

**7.**

(a) *Eleza katika sentensi maana ya misemo ifuatayo*

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(i) Uso wa chuma
(alama 1)

(ii) Kuramba kisogo
(alama 1)

(b) *Andika visawe (manenozyenye maana sawa) vya maneno haya;*

(i) Sarafu ............................... (alama 1)

(ii) Kejeli................................
(alama 1)

(iii) Daktari............................... (alama 1)

(c) *Kwa kila}ozi la maneno uliyopewa, tunga sentensi kutofautisha*

*maana* (i) Ini

Hini (alama 2)

(ii) tairi

tahiri (alama 2)

(d) Andika kinyume cha

(i) Shari ................................. (alama 1)

(ii) Oa...................................
(alama 1)

(e) (i) Anayefundisha mwari mambo ya unyumba huitwa
(alama 1)

(ii) Samaki anayejirusha kutoka majini huitwa (alama 1)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP**
**0705525657/0770195807**

8.

(a) *Tunga sentensi zitakazobainisha maana yajozi za maneno zifuatazo* (alama 4)

(i) Mbari Mbali

(ii) Kaakaa Gaagaa

(b) Tumia misemo ifuatayo katika sentensi (alama2)

(i) Enda nguu

(ii) Chemsha roho

(c) Eleza maana mbilitofautiza

Rudi (alama 2)

(d) eleza maana ya methali:

Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni

9. (alama 2)

(a) Tofautisha maana za sentensi zifuatazo:

i) Kazi yote ni muhimu.

ii) Kazi yoyote ni muhimu

(b) Eleza maana ya methali ifuatayo kwa kifupi: uji uki wa moto hupozwi kwa ulimi

(c) Eleza maana ya misemo ifuatayo

i) kukunjua jamvi______________________________ ii) kulamate ___

_______________________________

(d) Maana moja ya 'andika' ni kuchora maandishi ubaoni, kitabuni n.k

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Toa maana nyingine ya neno hilo (alamal)

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807